# UMBEA



**Tetesi**
Niliambiwa kwamba gharama ya vitu vinavyotengenezwa na Sign Industries ni kubwa.

**Jibu**
Inawezekana ni uvumi-hasi huo unaenezwa na makampuni tunayoshindana nayo kibiashara. Wivu katika biashara ni jambo la kawaida duniani kote. Hata hivyo, lazima tukiri kwamba sisi sio rahisi, kitu rahisi kina gharama zake.

Kamwe hatuwezi kupunguza bei ya bidhaa zetu, eti kwa sababu bei ya bidhaa za jirani yetu ni ndogo.

Sign Industries hutumia malighafi zenye ubora wa juu kabisa katika kutengeneza bidhaa zake. Watumishi wetu wana utaalamu na weledi usio na mashaka. Aidha tunazalisha bidhaa zetu kwa kutumia vitendea-kazi vilivyo bora kabisa, teknolojia ya kisasa na programu za kompyuta. Vigezo hivyo, ndio msingi wa kutetea uhalali wa bei za bidhaa zetu.



**Tetesi**
Nimejulishwa kwamba kuna mpango wa kuuza kampuni yenu!

**Jibu**
Sign Industries ni kampuni inayomilikiwa na kuendeshwa na wanafamilia. Lengo lake ni kuwekwa katika orodha ya wadau kwenye soko la hisa ngazi ya kitaifa, hata kimataifa. Pia kumiliki mali zingine zinazoweza kutuongezea mapato. Mkakati huu unaweza kupaisha hadhi yetu kiuchumi, hata nje ya mipaka ya nchi yetu.



**Tetesi**
Kuna uvumi kwamba Sign Industries huajiri wataalamu wa kigeni tu kushika nafasi za juu.

**Jibu**
Sera-mama ya Sign Industries ni kutoa fursa kulingana na utaalamu wa mtu. Vigezo vya kuajiri mtu ni: sifa yake kielimu, ujuzi, umahiri, pamoja na kuzingatia maadili ya utumishi. Hata hivyo, Watanzania hupewa kipaumbele.

Siku hizi, maombi ya kazi kwenye kampuni yetu, yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya mtandao. *(Rejea sehemu ya Fursa za Ajira).*



**Tetesi**
Watu wanasema kwamba bei ya bidhaa zinazozalishwa na kiwanda chenu ni za juu sana, wala hamtoi punguzo

**Jibu**
Sisi hukokotoa bei zetu kwa kutumia fomyula maalumu /au taratibu za kimahesabu. Kamwe hatupandishi bei ili kuwadanganya wateja kwa kutoa punguzo. Hata hivyo, mara nyingi tunatoa punguzo ili kuimarisha urafiki. Inapobidi, punguzo letu hutolewa kwa Pesa Taslimu.



**Tetesi**
Halo! Sina uhakika, ila kuna uvumi kwamba bosi wa Sign Industries Bw. Ismail amestaafu.

**Jibu**
Halo! Mimi bado ni bosi wa Sign Industries, sina wazo la kustaafu nikiwa bado hai. ☺
Ila subiri siku ya kufunikwa kwa udongo futi sita chini ya ardhi.

Hata hivyo, nimeanzisha mchakato wa kukaimisha baadhi ya majukumu yangu, ili nibaki na suala la Mahusiano na Umma, na Mashauriano. Majukumu yangu mengine niwaachie vijana walioelimika zaidi, wenye nguvu, shauku na ari ya kukabili mazingira-shindani ya kibiashara.



**Tetesi**
Kuna uvumi kwamba Sign Industries ina mapungufu / hitilafu katika sera zake za Bima

**Jibu**
Sign Industries inazo sera-rafiki kadhaa zinazohusu malipo ya Bima. Kampuni hii inao uwezo wa kumlipa mstahiki wa bima, hadi Shilingi Milioni 100,000,000. Vilevile tunakata bima kwa ajili ya mizigo inayosafirishwa hadi nje ya Tanzania. Tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi mkubwa. Hatuna mzaha katika kazi tunazozifanya.



**Tetesi**
Inasemekana kwamba Sign Industries hawatengenezi baadhi ya bidhaa kwa misingi ya kimaadili. Kwa mfano: Vileo, kasino, kamari, nakadhalika.

**Jibu**
Ni kweli, hatutaki kutumiwa kama chombo cha kuchochea tabia zisizokubalika katika jamii. Huu ndio msimamo wetu, mintarafu maadili.



**Tetesi**
Hebu tazama kihoja hiki!
Jina la kampuni **"Sign Industries"** linaashiria watengenezaji wa nembo/michoro /mabango. Ama sivyo? Lakini pia wanatengeneza bidhaa zingine nyingi ambazo hazina uhusiano na michoro. Haaaa!!! Hiki sikihoja?

**Jibu**
Huu ni ukweli kabisa. Unaweza kuona aina nyingi za bidhaa zetu kwenye chumba maalumu cha maonesho. Tunajivunia timu ya wafanyakazi wenye weledi mkubwa, na uzoefu wa kimataifa. Baadhi yao ni wamebobea katika fani za uinjinia na ujenzi kwa kutumia teknolojia ya kijiditali. Tunao uwezo mkubwa wa kusanifu na kutengeneza aina mbalimbali za bidhaa ambazo wateja wetu wanatoa oda mapema kulingana na mahitaji yao. Mathalani: bati za metali, vitu vya mbao, samani za ofisini na nyumbani, vifaa sanisi (synthetics), nakadhalika. Sampuli za vitu hivi vyote unaweza kuziona kwenye chumba cha maonesho.




**Tetesi**
Siku hizi baadhi ya makampuni yanazalisha bidhaa ambazo ni bora zaidi kuliko zenu

**Jibu**
Kwanza kabisa, hatujawahi kuchukulia makampuni mengine kama washindani wetu. Kwa sababu tunaamini kwamba ingawa soko ni moja, kila kampuni ina wateja wake, na kudura yake.

Pili, hatubezi bidhaa zinazotengenezwa na makampuni mengine, kufanya hivyo kutatia doa maadili yetu na taaluma yetu.

Tatu, ninasikitika kusema kwamba, makampuni mengi yanayotengeneza nembo na michoro nchini Tanzania, yana tabia ya kupora watumishi wetu ambao tunagharamia utaalamu wao. Huwashawishi wataalamu hao kwa nyongeza kidogo ya mshahara. Kwa hiyo, badala la kusikitika, tumejenga tabia ya kupuuzia vitendo viovu vinavyofanywa na makampuni ya aina hiyo. Tutaendelea kufundisha watumishi wapya, na kuwasimamia kwa makini.



**Tetesi**
Kuna uvumi kwamba Sifa za Waombaji wa kazi, kamwe hazimshawishi Meneja Rasilimali Watu kutoa uamuzi.

**Jibu**
Ni kweli. Wala hatuombi radhi kwa hili. Kwa sababu sisi huajiri watu, wala sio sifa zilizoandikwa kwa ustadi mkubwa kwenye karatasi.
Baadhi ya maombi hunakshiwa kupitiliza, lakini wanaoajiriwa hawafikii matarajio yetu. Uwezo wao kiutendaji hautoshelezi, pia hawajiamini.
Siku hizi, maelezo binafsi ya wanao omba kazi (CVs) yanaweza kunakiliwa kwenye mitandao. Kwa sababu hii, tunapendelea mahojiano ya ana kwa ana ili kubaini uwezo wao kwa vigezo tulivyoviweka.
Fomu tuliyoiandaa kwa ajili ya wanao omba kazi, inagusa vipengee vyote muhimu, na iko kwenye mtandao. Ikijazwa kwa ufasaha, inajitosheleza kabisa.
Kwa taarifa yako: Maelezo binafsi ya mwombaji yasizidi kurasa mbili. Mwombaji ajieleze bila kupinda-pinda. Asiwe na sifa ya kuwa mjuaji wa kila fani, na kutangatanga kwa waajiri kibao.